

LEARNING BY EAR 2009

Economics – 7th episode

SUCCEEDING IN THE BUSINESS WORLD

Series: “THE STORY OF TWO YOUNG PEOPLE, WHOSE SUCCESS STEMS FROM THEIR POCKET MONEY”

Author: Frédéric GAKPARA

Editors: Yann Durand and Sandrine Blanchard

Translator: Anne Thomas

KISUAHELI: Eric Ponda

SEVENTH EPISODE: "The first container"

Characters : **John** (*18-year-old boy, twin.*)
Jane (*John's twin sister.*)
Mr Ludovic (*32-year-old man, chief warehouse operator.*)
Mlle Ayawa (*28-year-old woman, decorator.*)
The workers (*Men and women employed by company.*)
Security agent (*44-year-old porter.*)
1st customs officer (*42-year-old man.*)
Head customs officer (*53-year-old man.*)
Shipowner (*38-year-old man, port agent.*)
Narrator

Learning by Ear Soundtrack

Intro

NARRATOR: Ni mara nyingine msikilizaji tunapoungana tena kwa makala nyingine ya mfululizo wa vipindi vya “Learning by Ear” Noa Bongo Jenga maisha yako vinavyotayarishwa na Deutsche Welle ,mada kuu ikiwa ni masuala ya Uchumi. Bado tunaendelea na hadithi ya Vijana wawili Mapacha ambao ufanisi wao Kiuchumi unatokana na juhudi zao za kuweka akiba ya sehemu ya pesa zao za matumizi. Sasa ni miezi miwili tangu John na Jane wapate mkopo wa benki. Tayari wanajiandaa kusafirisha kwa meli shehena ya kwanza ya Kampuni yao ya “Appetizers of the Tropics”.Ni katika bohari moja ambako jumla ya wafanyi kazi 23 wanamsaidia Jane kutayarisha shehena hiyo. Karibu kwa makala haya “**Shehena ya Kwanza**”

Scene 1, AT THE WAREHOUSE

JANE, MR LUDOVIC, MISS AYAWA, THE WORKERS...

ATMO: *Sounds of machines at the bag factory, sounds of plastic and glass bottles being put into boxes. Boxes being taped up. Workers talking to each other, giving each other instructions, laughing etc.*

- Jane:** Sikilizeni tafadhali! Leo tunashughuli nyingi kwa hivyo kila mmoja amakinike na kile anachofanya.Lazima tukamilishe shughuli hii

kabla ya saa kutimu. Lori haliwezi kutusubiri, na ni lazima mzigo huu ufike bandarini saa sita. Tayari Bw John anatusubiri na tayari amekamilisha kujaza fumo zote na stakabadhi nyingine za kusafirisha mzigo.. Shehena hii inatakiwa kupakiwa Melini saa Nane. Mnanielewa.?

2. **Workers:** Ndio Bi Jane!
3. **Jane:** Bw Ludovic?
4. **Mr Ludovic:** Ndio nakuelewa Bi Jane?
5. **Jane:** (*Aside*)
Na mhakikishe kuna kizibo kati kati ya chupa na sanduku kabla ya kulifunga ili kuzuia chupa zisivunjike .Hatuwezi kugharamia hasara hiyo. Tafadhali uwaambie wenzako wafanye upesi tafadhali tusichelewe.
6. **Mr Ludovic:** Tutafanya bidii na kila kitu kitakuwa shuari Bi Jane usiwe na wasi wasi.
7. **Jane:** Sawa....! Bi Ayawa?
8. **Mlle Ayawa:** Naam Bi Jane,. nimekuja.

- 9. Jane:** Nimeona tofauti kubwa baina ya nembo zilizochapishwa na kampuni na zile ulizotengeneza. Zile za kwanza zilikuwa nzuri lakini hizi tutazirudisha tafadhali!
- 10. ATMO:** *Jane's mobile phone rings. She answers.*
- 11. Jane:** Hallo , hallo John? Subiri kidogo! (*to Miss Ayawa*)
Kumbuka wakati shehena yetu itakapowasili Ulaya, na kuingia katika SuperMarket utakuwa ni wakati wa sherehe za mwisho wa mwaka . Jaribu kutumia ujuzi wako na ufanye haraka! Unaweza kwenda sasa!
(*to John*)
Sizungumzi na wewe , nilikuwa na zungumza na Bi Ayawa... Hakuna shida kila kitu ni sawa. Ni mabadiliko kidogo tu kuhusu nembo. Vipi mambo yanaendeleaje huko? Anataka ngapi? Hatuna budi....! huu ni ulimwengu wa mbio kama Baba anavyotuambia kila wakati! Tutamaliza katika muda usio mrefu. Lori litafika hapa mwendo wa saa tano, na tunataka tufanye haraka iwezekanavyo, nadhani tutafika bandarini kwa wakati ufao. Tuonane baadaye Kwaheri....!

12. ATMO: *The factory sounds fade. Music marks the passing time...*

NARRATOR: Lori linafika katika bohari likia limejazwa masanduku ya Njugu zilizo karangwa na kutiwa chumvi, Njugu tamu zilizotiwa sukari, Unga wa Nujgu karanga na machicha ya nazi na bidhaa nyingine . John tayari anasubiri na stakabadhi zote za uafirishaji.

Scene 2, AT THE PORT

JOHN, JANE, SECURITY AGENT, 1st CUSTOM'S OFFICER, HEAD CUSTOM'S OFFICER, SHIPOWNER

13. ATMO: *Sound of lorry stopping with engine still running. Jane climbs out. We hear the door open and close. The port is very busy. Workers, dockers, shopkeepers and people going to and fro.*

14. Jane: Kila kitu ni sawa ?

15. John: Ndio nimepata stakabadhi zote za usafirishaji.

16. Jane: *(To the security agent)*
Habari Bw!

17. **Security agent:** Nzuri !
18. **John:** (*To the security agent*)
Hili ndilo Lori...
19. **Security agent:** HmMMM!
(*To his colleague*)
Lazima tulifungue!
20. **ATMO:** *The barrier opens with a big squeak. The lorry moves forward and stops in front of the customs. The engine cuts. John and Jane walk to the lorry.*
21. **1st custom's officer:**
Hii ni mali yenu?
22. **John:** Ndio chifu !
23. **1st custom's officer:**
Ni nyingi sana, Kisheria tunapasa kufungua
na kutazama kila kitu ndani ya Lori.
(*He walks around the vehicle*)
24. **John:** Kweli ?

- 25. 1st custom's officer:**
Ndio ... lakini kama mna haraka mnaweza kwenda kuzungumza na mkubwa pale.
- 26. Jane:** (*Whispering to John*)
John, anachotaka ni hongo!
- 27. John:**
Naelewa mchezo wao. Wote hawa ni mafisadi!
- 28. Jane:**
Kama hatutatoa kiinua mgongo hapa watafungua masanduku yote baada ya juhudi zetu za kufunga na kuweka sili.,.,.,
- 29. 1st custom's officer:**
Kwa hivyo tufanyeje ndugu zangu?
Tuyafungue?
- 30. John:**
Boss yuko wapi?
- 31. 1st custom's officer:**
Nitawapeleka katika ofisi yake. Makaratasi yote ya usafiri ni sawa. Mtamueleza tu kwamba ni Njugu na kwamba
- 32. ATMO:** *The boss arrives. The custom's officer stands to attention*

33. 1st custom's officer:

Boss, hawa wanasafirisha njugu. Lori lao ni lile pale.

34. Chief custom's officer:

Makaratasi yote ni sawa?

35. 1st custom's officer:

Ndio Boss, lakini masanduku yote yamefungwa na kuwekwa sili.,...

36. Chief custom's officer:

Ni masanduku mangapi?

37. Jane:

Ni masanduku 200.

38. Chief custom's officer:

Sawa, kila sanduku ni faranga 100 kwa jumla mtalipa faranga elfu 20.

39. John:

Lakini Boss sina pesa utachukua faranga elfu 10?

40. Chief custom's officer:

La sivyo tuyafungue masanduku yote.. sawa?.

- 41. Jane:** Samahani Boss siku nyingine tutalipa ada yote, Tumetumia pesa zote kwa biashara hii. Tutarudi siku nyingine... tafadhali??
- 42. Chief custom's officer:**
Huyu ni Kakako?
- 43. Jane:** Ndio Boss.
- 44. Chief custom's officer:**
Nipe hizo faranga elfu 10!
- 45. John:** (*He looks for it*)
Ndio hizi Boss!
- 46. Jane:** Asante Boss!
- 47. ATMO:** *We hear their steps going back to the lorry.*
- 48. Chief custom's officer:**
(*To Jane*)
Msichana, na uwe ukitutembelea mara kwa mara !
- 49. Jane:** Sawa Boss!

- 56. Jane:** Muhimu ni shehena ifike salama. Kila changamoto inatufunza funzo fulani.
- 57. John:** Dereva tunaweza kuliegesha hapa. Ofisi ya mwenye meli ni hii hapa
- 58. ATMO:** *The car stops and the engine cuts. Sound of the door. John goes to towards the office, followed by Jane.*
- 59. Shipowner:** *(From a distance)*
Tunawasubiri nyinyi... Bw John!
- 60. John:** Tumekamilisha. Shehena iko ndani ya Lori.
- 61. Shipowner:** *(Coming towards the lorry, calling from a distance...)*
Abass! waite hao wengine tupakue mzigo huu mara moja.
- 62. John:** Meli itaondoka leo?
- 63. Shipowner:** Tayari shughuli ya ukaguzi inaendelea. Siku hizi imekuwa gharama meli kutia nanga katika bandari hii.
- 64.**

65. Punde tu shughuli ya ukaguzi itakapo kamilika tutang'oa nanga kuepukana na gharama zaidi.
66. **Jane:** Itawachukua siku ngapi kuwasili Hamburg?
67. **Shipowner:** Siku 25 hivi ,...John huyu ni Dada yako?
68. **John:** Ndio.
69. **Shipowner:** Ni mrembo sana ?
70. **John:** Asante !
71. **Shipowner:** (*To the dockers*)
Hebu pakieni mizigo kwa kontena(*To John*)
Kisha muyapime kabisa tujua gharama yake.
72. **John:** (*To the ship owner*)
Utuhurumie Bwana!
73. **Shipowner:** Usijali John, kila kitu kitakuwa sawa, hebu nifuate !
74. **ATMO:** *John and the ship owner's steps towards the office. Jane hums a **sad song**. The ship sounds?. John runs towards Jane who is crying.*

75. John: Ni nini Jane? Kila kitu ni sawa. Tayari mzigo wetu umepakiwa!

76. Jane: (*crying*)
Hata si hivyo.... Si kitu. Nina wasi wasi ni pesa ngapi tutakazoendelea kutumia ili kufanikisha malengo yatu

NARRATOR: Kama ulivyosikia mambo si rahisi kusafirisha shehena kwa meli hadi ng'ambo Lakini huwezi kuvuna bila ya kutoa jasho. Jane na kakake John wamekumbana na vikwazo vya aina mbali mbali lakini hatimaye wamefauli kufikisha mzigo Bandari. Na kilio cha Jane ni kutokana na fedheha ya muda mrefu!

77. Closing soundtrack to be left running after the outro and brought up

NARRATOR: Lakini nini kitakachotokea baada ya kusafirisha shehena yao ya kwanza? Ili kujua mengi zaidi ungana nasi kwa kipindi kijacho katika mfululizo wa vipindi vya "Learning By Ear" Kumbuka pia unaweza kukisikiliza tena kipindi hiki au ukiwa na maoni usisite kututumia kupitia mtandao wa **dw-world.de / I b e**. Hadi wakati mwengine kwaheri kwa sasa!

Music up

END